



## Usalama wa Chanjo za COVID-19

### Kile unachohitajika kujua

- Chanjo za COVID-19 ni **salama na faafu**.
- Mamilioni ya watu Marekani wamepokea chanjo za COVID-19 chini ya ukaguzi wa dharti zaidi wa kiusalama katika historia ya Marekani.
- Kituo cha CDC kinapendekeza upate chanjo ya COVID\_19 punde iwezekanavyo.
- Watu wengi wameripoti tu madhara madogo baada ya kuchanjwa dhidi ya COVID-19.

### Mamilioni ya watu wamepokea chanjo ya COVID-19 kwa njia salama

Zaidi ya dozi milioni 272 za chanjo ya COVID-19 zimetolewa Marekani kuanzia tarehe 4 Disemba, 2020 hadi tarehe 17 Mei, 2021.

Chanjo za COVID-19 ni **salama na faafu**. Chanjo za COVID-19 zilitathminiwa katika makumi ya maelfu ya washiriki katika majaribio ya kimatibabu. Chanjo zilitimiza viwango vikali vya usalama, ufaafu na ubora wa utengenezaji vya asasi ya kusimamia vyakula na madawa (FDA) vinavyohitajika kuwezesha kutolewa kwa kibali cha matumizi ya dharura. [Learn more about EUAs in this videoexternal icon.](#) (Jifunze zaidi kuhusu Kibali cha Matumizi ya Dharura kuitopia kitufe hiki)

Mamilioni ya watu nchini Marekani wamepokea chanjo za COVID-19 tangu zilipoidhinishwa kwa matumizi ya dharura na asasi ya FDA. Chanjo hizi zimepitia na zitazidi kuitopia ukaguzi wa dharti zaidi wa kiusalama katika historia ya marekani. Ukaguzi huu unahusisha matumizi ya mifumo mipyaa pamoja na ile iliyotumiwa kwa muda mrefu ya ukaguzi ili kuhakikisha kwamba chanjo za COVID-19 ni salama.



## Matokeo yanaondoa mashaka

Matokeo kutokana na juhudzi za ukaguzi wa usalama wa chanjo yanaondoa mashaka. Baadhi ya watu hawapati madhara yoyote. Wengine wameripoti madhara ta kawaida [side effects after COVID-19 vaccination](#). (Madhara baada ya kupata chanjo ya COVID-19) kama vile:

- Uvimbe, wekundu, na maumivu katika eneo lililodungwa
- Joto la homa
- Maumivu ya kichwa
- Uchovu
- Maumivu ya misuli
- Homa ya baridi
- Kichefuchefu

### Matatizo ya dhati ya kiusalama ni nadra

Kufikia sasa, mifumo iliyowekwa kukagua usalama wa chanjo hizi umepata aina mbili tu za matatizo ya dhati baada ya kuchanjwa, yote mawili ni nadra. Matatizo hayayanajumuisha anaphylaxis (mzio mkali) na thrombosis with thrombocytopenia Syndrome - TTS (kuganda kwa damu katika mishipa) baada ya kupokea chanjo ya COVID-19 ya J&J/Janssen.

### Mzio Mkali

Idadi ndogo ya watu wamekuwa na [severe allergic reaction](#) mzio mkali (unaoitwa "anaphylaxis") baada ya kuchanjwa lakini tukio hili ni **nadra**. Mzio mkali unaweza kutokea baada ya kupata chanjo yoyote. Iwapo hali hii itatokea, wanaotoa chanjo wana dawa zilizopo za kutibu hali hii mara moja ipasavyo.

Baada ya kupata chanjo ya COVID-19, utaambiwa usubiri kwa baina ya dadika 25 na 30 ili uangaliwe iwapo una mzio mkali utakaotokea na kuhitaji matibabu ya papo hapo.

**kuganda kwa damu katika mishipa (Thrombosis with Thrombocytopenia Syndrome - TTS) baada ya kupokea chanjo ya COVID-19 ya J&J/Janssen**



Baada ya kupokea chanjo ya COVID-19 ya J&J/Janssen, kuna hatari ya tukio nadra lakini hatari - vidonge vya damu vilivyo na chembelele chache (thrombosis with thrombocytopenia syndrome, au TTS). Wanawake walio chini ya umri wa miaka 50 hasa wanapaswa kutambua hatari ya juu ambayo inawakumba kutokana na tukio hili nadra lakini hatari. Kuna chanjo nyingine za COVID-19 zinazopatikana na ambazo kwazo hatari hii haijatokea.

Tukio hili kali ni nadra, linatokea katika kiwango cha wanawake 7 kati ya wanawake milioni 1 waliochanjwa na walio na umri wa baina ya miaka 18 na miaka 49. Kwa wanawake walio na umri wa zaidi ya miaka 50 na wanaume wa umri wowote, tukio hili kali ni nadra hata zaidi.

## **Madhara ya muda mrefu hayatarajiwi.**

Madhara makali ambayo yanaweza kusababisha matatizo ya muda mrefu ya kiafya hayatarajiwi kutokana na chanjo yoyote ikiwemo chanjo za COVID-19. Ukaguzi wa chanjo kihistoria umedhihirisha kuwa madhara aghalabu hutokeea ndani ya majuma sita baada ya kupokea chanjo. Kwa sababu hii, asasi ya FDA ilielekeza kwamba kila chanjo iliyoidhinishwa kutumiwa ifanyiwe utafiti kwa angalau miezi miwili (majuma nane) baada ya kupata dozi ya mwisho. Mamilioni ya watu wamepokea chanjo za COVID-19, na hakuna madhara ya muda mrefu ambayo yamegunduliwa.

Kituo cha CDC kinaendelea kukagua kwa makini usalama wa chanjo za COVID-19. Iwapo wanasayansi watapata uhusiano baina ya suala la kiusalama na chanjo, asasi ya FDA na kampuni inayotengeneza chanjo husika watashirikiana katika kutafuta suluhu faafu ili kushughulikia shauku hiyo ya kiusalama (kwa mfano, tatizo la fungu fulani, suala ya utengenezaji, au chanjo yenyewe).



## Saidia kujikinga na kuwakinga wengine kwa kuchanjwa

Kuchanjwa dhidi ya COVID-19 na kufuata [CDC recommendations on wearing masks and social distancing](#) (mapendeleko ya CDC kuhusu kuvala barakoa na kudumisha umbali) ni njia bora zaidi za kujikinga dhidi ya COVID-19. Kituo cha CDC kinapendekeza upate chanjo ya COVID-19 haraka iwezekanavyo.

Kituo cha CDC, asasi ya FDA na asasi nyingine za jumuia zitaendelea kukagua usalama wa chanjo za COVID-19 kadri zinavyotolewa kwa wingi mionganoni mwa watu.